



# FAHARI YETU

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

TOLEA

LA PILI

OKTOBA HADI

DESEMBA

2022



ASANTE DK.SAMIA SULUHU HASSAN

KUTOA MILIONI 340 ZA  
UJENZI WA NYUMBA 17  
VYA MADARASA,  
WANAFUNZI WA KIDATO  
CHA KWANZA MWAKA  
2023 WAMENUFAIKA NA  
VVUMBA VIPYA VYA  
KISASA VYA MADARASA  
NA SAMANI ZAKE (VITI NA  
MEZA)



@merudc



merudistrictcouncil2



www.merudc.go.tz

# Wanafunzi 6,914 wa kidato cha kwanza 2023 Wanufaika



Serikali ya awamu ya sita inayo ongozwa na Dkt.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuboresha sekta ya Elimu nchini ikiwa ni mkakati wa kuhakikisha elimu bora inaendelea kutolewa kwa watoto wakitanzania katika mazingira yaliyoboreshwa, ambapo imeendelea kutoa fedha za uboreshaji wa miundombinu ya kujifunzia na kujifunzia katika katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023 imetoa shilingi milioni 340 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 17 vya madarasa katika shule 13 za Halmashauri ya Wilaya ya Meru ambavyo vimekamilia pamoja na asamani zake (viti 50 na meza 50 kwa kila darasa).

Aidha Wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023 katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, ni wanufaika na vyumba hivi vipya na vya kisasa vya madarasa pamoja na samani zake wameishukuru serikali Serikali ya awamu ya sita inayo ongozwa na Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuwaboresha mazingira ya kujifunzia ambapo wameahidi kusoma kwa bidii "tunamshukuru Rais wetu Dkt.Samia kwa kutujengea madarasa mazuri yametuvutia sanayana vigae,viti na mezaumeme nk "" Ameeleza rubeni robert mwanafunzi wa kidato cha kwanza shule ya sekondari majengo

MERU  
TUMENUFAIKA  
TUNASHUHEDIA  
MAENDELEO  
YANAYOFANYWA  
NA AWAMU  
YA SITA  
KAZI IENDELEE....



# Wazazi Halmashauri ya Wilaya Meru Waishukuru Serikali kuwaondolea adha ya michango



wazazi na walezi katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, wameishukuru Serikali ya Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha sekta ya Elimu ambapo kwa sasa wamepungiziwa mzigo wa michango kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa "tunafarijika kuona watoto wanasoma katika mazingira mazuri kwani mbali na serikali kujenga vyumba vya madarasa imetoa fedha za viti na meza" ameeleza Samweli Kinga mkazi wa Usa-River wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa vyumba vya madarasa iliyoongozwa na Mhe.John Mongela, Mkuu wa mkoa wa Arusha.

Shukrani hizi ni muendelezo wa mrejesho wa wananchi kwa serikali kwa uboreshaji mkubwa na wenye tija unaofanywa na serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ambapo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilitoa Shilingi Bilioni 1.4 fedha za UVIKO - 19 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 70 vya madarasa pamoja na samani zake (viti 50 na meza 50 kwa kila darasa) katika shule 33 za Halmashauri ya Wilaya.Ujenzi huu wa vyumba 70 vya madarasa vimepelekea serikali ya awamu ya sita kuweka historia kwa mara ya kwanza wanafunzi wote wahitimu wa elimu ya msingi na waliochaguliwa kjiunga na kidato cha kwanza kuripoti kwa awamu moja tofauti na kipindi cha nyuma ambapo walipangwa kwa awamu takribani tatukutokana na kutokana na uhaba wa vyumba vya adarasa katika shule za sekondari.

ELIMU  
BORA  
KWA KILA  
MTOTO  
WA  
KITANZANIA

KAZI IENDELEE.....



## MKUU WA MKOA WA ARUSHA ARIDHISHWA NA VIWANGO VYA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA



Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongela ameipongeza Halmashauri ya Meru, Wilayani Arumeru kwa ukamilishaji wa vyumba 17 vya madarasa katika shule 13 za Sekondari ambapo amebainisha vyumba hivyo kuongoza kwa kiwango cha ubora kati ya Halmashauri zote saba za Mkoa huo.

Mhe. Mongela amesema hayo katika hafla fupi ya makabidhiano ya Vyumba hivyo 17 iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Muungano, ambapo ametoa wito kwa viongozi ndani ya Mkoa huo kujituma na kushirikiana ili kufikia azma ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwaletea wananchi Maendeleo " tunaona ufuatiliaji na ushirikiano uliopo kati ya Serikali, Chama na wananchi, Meru mmefanya vizuri hongereni sana "amepongeza Mhe. Mongela

Akisoma taarifa, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl. Zainabu Makwinya amesema Halmashauri hiyo ilipokea Milioni 340 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 17 vya madarasa na samani zake (viti 50 na meza 50) katika shule 13 za Sekondari ambapo amemshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani vyumba hivyo vitawanufaisha wanafunzi 6,914 wa kutwa waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023.

Awali, Mhe. John Mongela amesema uboreshaji wa sekta ya elimu unaofanywa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unalenga kutoa elimu bora kwa kila mtoto wa kitanzania ambapo ameelekeza wanafunzi wote wa kidato cha kwanza mwaka 2023 kuripoti shule tarehe 09 Januari 2023 bila kuchelewa, sambamba na viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza darasa la awali na la kwaza wanaandikishwa.

# MWENYEKITI WA CCM MKOA WA ARUSHA ARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM MERU, kazi iendeleee



viongozi wa Chama wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha Mhe. Zelothe Steven Zelothe, wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa vyumba 17 vya madarasa, wamempongeza Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kutekeleza Ilani ya chama hicho, inayolenga kuwaletea wananchi maendeleo kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia





Mhe. Jeremia Kishili  
Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Meru

MERU TUPO VIZURI  
UBORESHAJI SEKTA YA  
ELIMU SEKONDARI,  
MSINGI NA AWALI  
KAZI IENDELEE




Mwl. Zainabu J. Makwinya  
Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Meru

### Serikali yatoa Shilingi Milioni 485 za uboreshaji miundombinu Elimu Msingi

SERIKALI IMEENDELEA KUWAHAKIKISHIA WANANCHI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU UPATIKANAJI WA ELIMU BORA KWA KILA MTOTO WA KITANZANIA AMBAPO IMETOA MILIONI 485 KWAAJILI YA UJUNZI WA MIUNDOMBINU MBALIMBALI.

AIDHA KATIKA FEDHA HIZO MILIONI 485 KIASI CHA MILIONI 200 NI ZA UJENZI WA NYUMBA NNE (2 IN 1) ZA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI LOSITETE, KWATULELE, MIEMBENI NA OLTEPESI AMBAPO KILA NYUMBA ITAGHARIMU KIASI CHA SHILINGI MILIONI 200

VILEVILE KATIKA FEDHA HIZO MILIONI 485 KIASI CHA SHILINGI ZITATUMIKA KATIKA UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU KARIKA SHULE KONGWE TATU MADARASA AMBAPO KILA SHULE IMEPATA SHILINGI MILIONI 60 ZA UJENZI WA VYUMBA VITATU VYA MADARASA PAMOJA NA SAMANI ZAKE KWA KIASI CHA MILIONI 20 KWA KILA DARASA HIVYO JUMLA KUU KWA SHULE ZOTE KUWA MILIONI 180.



Muonekano wa chumba cha darasani awali katika shule ya Msingi Manyata



chumba cha darasa katika shule ya Msingi kikwe ni miongoni mwa vyumba 9 katika shule kongwe ambavyo serikali ilitoa milioni 180 za ujenzi



## WAZIRI JENISTA AZIELEKEZA HALMASHAURI ZA MERU NA ARUSHA KUWAENDELEZA WATUMISHI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista Mhagama amezitaka Halmashauri za Meru na Arusha Wilayani Arumeru kuwabadilishia miundo watumishi sambamba na kutenga bajeti za kuwaendeleza watumishi waliopo ili kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi .

Waziri Mhagama amesema hayo wakati akizungumza na Watumishi wa Halmashauri za Meru na Arusha Wilayani Arumeru, ambapo amebainisha ubunifu ni muhimu katika kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi uliopo.

Vilevile Mhe.Mhagama amehimiza haki za watumishi kupewa kipaumbele sambamba na kuwa na usawa kwa watumishi katika fursa na uwezeshaji toka Serikalini ili watumishi wajisikie na kujivunia kuwa sehemu katika kujenga nchi hii "niwatake Wakurugenzi kuhakikisha watumishi wa kada zote wananufaika na fursa za Serikali ya awamu ya sita pamoja na kuhakikisha watumishi wanapewa haki zao na kutatuliwa changamoto walizo nazo kwa wakati"amehimiza Mhe.Waziri Mhagama.

Mhe.Mhagama amesema Serikali imewekeza sana kwa watumishi wa umma, ambapo ametoa wito kwa Watumishi kuweka malengo na kuyatekeleza ambapo amehimiza haki kuenda sambamba na wajibu.

Pia. Mhe.Waziri Mhagama amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya kwa ujazaji wa taatifa za watumishi kwenye mifumo ambapo Halmashauri hiyo imefika zaidi ya asilimia 96%.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe .John Mongela amesema mafanikio katika sekta mbalimbali za Mkoa wa Arusha ni pamoja na mchango wa watumishi, ambapo ameahidi Mkoa kutekeleza maagizo na ma maelekezo yote ya Mhe.Waziri



#### MERU TUMENUFAIKA AWAMU YA SITA KAZINI

serikali imeendelea kuboresha maslai ya watumishi katika halmashauri hiyo ambapo kwa kipindi cha mwaka mmoja imetoa mkopo usio na riba kwa watumishi wa Halmashauri hiyo kiasi cha Shilingi milioni 600 kuwawezesha kununua vyombo vya usafiri

**KAZI IENDELEE.....**

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya akiwasilisha taarifa ya Watumishi amesema serikali imeendelea kuboresha maslai ya watumishi katika halmashauri hiyo ambapo kwa kipindi cha mwaka mmoja imetoa mkopo usio na riba kwa watumishi wa Halmashauri hiyo kiasi cha Shilingi milioni 600 kuwawezesha kununua vyombo vya usafiri, sambamba na kutoa ajira kwa watumishi 133 wa kada mbali mbali,kupandisha madaraja watumishi 1,245 ambapo amebainisha bado kunaupungufu wa watumishi 696 wa sekta mbali mbali.





Wakuu wa Idara/Vitengo, Halmashauri ya Wilaya ya Meru wakati wa kikao na Mhe. Waziri Jenista Mhagama



Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru wakati wa kikao na Mhe. Waziri Jenista Mhagama



Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru wakati wa kikao na Mhe. Waziri Jenista Mhagama

## WAZIRI KAIRUKI ATOA ANGALIZO UTEKELEZAJI MRADI WA BOOST



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Angella Kairuki amesema hatasita kuwachukulia hatua stahiki kwa wale wote watakaovuruga, kufuja fedha za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Shule za Awali na Msingi kwenye utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Awali na Msingi (BOOST)

Ameyasema hayo leo tarehe 13 Disemba, 2022 wakati akifungua Mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa timu za utekelezaji wa mradi wa BOOST katika Mikoa ya Singida, Manyara na Arusha, uliofanyika katika ukumbi wa shule ya Sekondari ya Ilboru mkoani Arusha.

“Serikali inapimwa kwa vigezo katika kutekeleza Mradi wa BOOST nchini sitakuwa tayari kuona fedha zimetolewa kiasi cha shilingi trilioni 1.15 na kupelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa lakini miradi haitekelezwi kwa wakati na fedha hizo kurudishwa, tutakuwa hatujatenda haki kwa wananchi” amesisitiza Waziri Kairuki

Waziri Kairuki amewataka Wajumbe wa mradi huo kuhakikisha fedha zinazotolewa katika utekelezaji wa miradi zinakamilisha miradi iliyopangwa ili kuepusha miradi mingi kutokukamilika huku fedha zikiwa zimekwisha

Amewataka wajumbe hao kuhakikisha wanaimarisha ushirikiano na jamii katika utekelezaji wa mradi na kutekeleza afua zote za mradi kwa wakati ukiwemo ujenzi wa miundombinu ili kufikia matokeo yaliyokubalika;

Aidha, amewaagiza Wajumbe hao kuwahamasisha wazazi/walezi kuwapeleka watoto wenye umri wa kuanza shule ili waandikishwe na kuanza shule kwa wakati ili kuwaepushia mzigo walimu wa kulazimika kurudia kufundisha mambo yale yale kutokana na wanafunzi wengine kucheleweshwa kuanza shule

# WAZIRI BITEKO AKUTANANA WACHIMBAJI WADOGO WA MADINI MERU WILAYANI ARUMERU



Waziri wa Madini Dkt. Dotto Biteko amesema Serikali ya awamu ya sita inaendelea kuhakikisha Wananchi wananufaika na madini kwa kutatua changamoto kwa wachimbaji wa madini wakubwa na wadogo ili wafanye kazi kwa amani na kushiriki kikamilifu kujenga uchumi wa nchi.

Waziri Biteko amesema hayo wakati wa ziara kwenye machimbo ya kokoto katika Kata ya Malula, Halmashauri ya Wilaya ya Meru ambapo ameitaka Kampuni ya Madini ujenzi ya Rocktronic Ltd inayochimba kokoto kuandaa mpango wa huduma kwa jamii inayozunguka mgodi huo ili kuiwezesha jamaii kunufaika na rasilimali madini iliyopo katika maeneo yake na kuondoa migongano inayoweza kujitokeza siku za baadae.

Vilevile Mhe. Biteko ameitaka kampuni hiyo kuandaa taarifa ya upembuzi yakinifu ili kuiwezesha kujua muda wa uhai wa mgodi, kiasi cha mashapo na kiasi kitakacholipwa kwa serikali sambamba na kutunza mazingira ambapo ametoa siku 14 kwa kampuni hiyo kuanza kupanda miti katika maeneno ya machimbo ili kuhifadhi mazingira.

Awali afisa Madini mkazi wa Mkoa wa Arusha Mhandisi Alphoce Bikulamchi ameeleza mkoa wa Arusha una migodi ya madini ya ujenzi yenye leseni ipatayo 18

Nao wawekezaji wa machimbo hayo wameahidi kutekeleza maagizo ya Mhe. Waziri pamoja na kuendelea kushiriki katika maendeleo kwa kulipa Kodi nk.

# WAZIRI KAIRUKI ATOA ANGALIZO UTEKELEZAJI MRADI WA BOOST



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Angella Kairuki amewaagiza Maafisa elimu Maalum wote nchini kuhakikisha wanasimamia zoezi la uchunguzi wa awali wa watoto ili kubaini watoto wenye mahitaji maalum katika jamii.

Ameyasema hayo leo tarehe 12 Disemba, 2022 wakati akifungua mafunzo kwa maafisa elimu watu Wazima na maafisa elimu Maalum iliyofanyika katika ukumbi wa chuo cha Ualimu Patandi, Mkoani Arusha.

Amewataka kuhakikisha wanatumia vituo vya uchunguzi (Education Support Resource Assessment Centre) na kuwaelekeza watoto wenye mahitaji maalum katika shule stahiki ambazo wanapaswa kupelekwa ili wapate afua stahiki

Waziri Kairuki ameelekeza shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu zihusishe kikamilifu masuala ya elimu maalumu na elimu ya watu wazima kwa kuhakikisha wanashirikiana na viongozi katika jamii katika kuratibu shughuli za elimu ya watu wazima na elimu Maalum katika shule za msingi na Sekondari

Ametoa rai kwa Maafisa hao kuweka utaratibu wa kupokea wanafunzi wenye mahitaji maalum wa kidato cha kwanza, darasa la kwanza na awali kwa mwaka 2023 kwa kushirikiana na viongozi katika maeneo yao ili kuweka mazingira bora kwa wanafunzi hao

Waziri Kairuki amewataka viongozi wa elimu katika ngazi ya shule, Kata, Halmashauri na Mikoa kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji shuleni na kushirikiana na walimu katika kuhakikisha wanafunzi wanapata umahiri uliokusudiwa badala ya kukaa ofisini.

Aidha, ameaagiza kila mwalimu lijiweke malengo binafsi katika masomo anayofundisha na kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayeshindwa kupata umahiri uliokusudiwa katika somo lake ifikapo mwishoni mwa kila mwaka



Halmashauri ya Wilaya ya Meru imekabidhi Hundi ya mfano yenye thamani ya Milioni 237 kwa vikundi vya Wanawake 36,Vikundi 18 vya Vijana na vikundi vinne vya watu wenye ulemavu.

Akizingunza wakati wa utoaji mikopo isiyo na riba ya asilimia 10% ya mapato ya Halmashauri Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mhe.Jeremia Kishili ametoa wito kwa vikundi hivyo kutumia fedha za mkopo kwa malengo yaliyokusudiwa"kinamama msitumie fedha hizi kununua nguo/vitenge, siku zote ili kupiga hatua kiuchumi mtu anapaswa kutumia faida na si mtaji" amehimiza kishili

Mhe.Kishili amesema utoaji wa mikopo isiyo na riba ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Sura ya Pili ibara 23 ambayo inalenga kuwawezesha wanawake ,Vijana na Wenye ulemavu kujikwamua kiuchumi "Serikali yetu ya chama cha Mapinduzi CCM inawajali na kuwathamini wananchi wote ndio maana imeweka sera zinazowanufaisha" amesema Kishili

Mhe.Kishili amewaasa Wanawake wanao nufaika na mkopo huo kuendelea kuwaheshimu kina baba majumbani ili fursa hiyo ya mikopo ikaimarishe uchumi wa familia na mahusiano "amesema Kishili

Vilevile Mhe. Kishili amepongeza mwamko wa vikundi vya vijana kuchangamkia fursa ya mikopo hiyo ambapo idadi ya vikundi vilivyopata mkopo imeongezeka kutoka vikundi 10 hadi 18 "tunawapongeza vijana baada ya elimu na hamasa mwitikio umeanza .Pia ni jambo jema wenye mahitaji maalum wananufaika pia na idadi inaongezeka baada ya Serikali kurahisisha masharti kwani sasa mtu mwenye changamoto ya ulemavu anaweza kukopesha mwenyewe" ameeleza Kishili




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mhe. Jeremia Kishili amesema Halmashauri hiyo itaendelea kukusanya mapato na kuwaletea wananchi maendeleo ambapo ametoa wito kwa waendasha pikipiki kuwa waadilifu na kutumia vyombo hivyo kujiletea maendeleo

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl. Zainabu Makwinya ametoa wito kwa vikundi vilivyonufaika na mkopo huo usio na riba kujikwamua kiuchumi kwa kuchapa kazi kwa bidii ili kuwa chachu ya maendeleo kwenye jamii "Serikali inahakikisha mbali na kuboresha miundombinu katika sekta mbalimbali mbali za afya, elimu nk inaboresha maisha ya wananchi wake kwa kuweka sera za kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na utoaji wa mikopo isiyo na riba" amesema Mwl. Makwinya



## MBUNGE WA ARUMERU MASHARIKI AKABIDHI PIKIPIKI 18 KWA VIJANA, MASHINE YA KUTOTOLEA VIFARANGA KWA WANAWAKE



Halmashauri ya Wilaya ya Meru imekabidhi vyombo vya usafiri (Pikipiki) 18 venye thamani ya shilingi Milioni 45 kwa vikundi vitatu vya vijana pamoja na mashine ya kutotolea vifaranga (incubator) yenye thamani ya shilingi Milioni 8 ikiwa nisehemu ya Mkopo kiasi cha milioni 237 uliotolewa na Halmashauri katika robo ya kwanza kwa mwaka huu wa fedha.

Akikabidhi Pikipiki hizo kwa vijana Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki Dkt. John D. Pallangyo ametoa rai kwa vijana kujikwamua kiuchumi kwa kutumia vyombo hivyo vya usafiri ikiwa ni pamoja na kuzitunza na kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuwa na afya njema kwa kuepuka ajali zitokanazo na uzembe.



**Mhe. Jeremia Kishili**  
Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Meru

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mhe. Jeremia Kishili amesema uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia ikopo isiyo na riba na utekelezaji wa miradikatika sekta za elimu, afya na kipaombele cha baraza la madiwani wa halmashuri hiyo, hivyo Halmashauri itaendelea kukusanya mapato na kutumia apato hayo kuwaletea wananchi maendeleo ambapo ametoa wito kwa waendasha pikipiki kuwa waadilifu na kutumia vyombo hivyo kujikwamua kiuchumi.

Vilevile kishili ametoa wito kwa wananchi kulipa tozo mbalimbali za Halmashauri kwani zinatumiwa kuwaletea maendeleo






Mwl.Zainabu Makwinya  
Mkurugenzi Mtendaji Halmahauri ya Meru

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Mwl. Zainabu Makwinya amesema ushirikiano uliopo kati ya waheshimiwa madiwani na wataalam umesaidia kuhakikisha mapato yanakusanywa na kutumika kuwaletea wananchi maendeleo kupitia utoaji wa mikopo isiyo na riba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo nk

Vilevile Makwinya ameeleza pamoja na Halmashauri kutoa mkopo wa Pikipiki kwa vijana na Mashine ya kutolea Vifaranga, lakini pia aliomba Ofisi ya waziri Mkuu vifaa kama cherehani kwa vijana ili wajiajiri na kujikwamua kiuchumi.

# HALMASHAURI YAWAWEZESHA WANANWAKE, YATOA MASHINE YA KUTOTOLEA VIFARANGA



Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki Dkt. John D. Pallangyo AKIKABmashine ya kutotolea vifaranga (incubator) yenye thamani ya shilingi Milioni 8

Awali, akisoma taarifa Afisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Meru Bi. Flora Msilu amesema vifaa hivyo vyenye thamani ya Milioni 53 ( pikipiki 18 na mashine ya kutotolesha vifaranga) vimenunuliwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri na ni sehemu ya Mkopo usio na riba kiasi cha Milioni 237 ambao umetolewa kwa vikundi vya Wanawake 36, Vikundi 18 vya Vijana na vikundi vinne vya watu wenye mahitaji maalum kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha 2022/2023.

# VIONGOZI WA CCM WAIPONGEZA MERU,WAHIMIZAUTOAJI WA MIKOPO KWA WANANCHI NI UTEKELEZAJI WA ILANI



Nao viongozi mbalimbali wa Chama cha mapinduzi wakiongozwa na katibu mwenezi Wilaya ya kichama Meru Ndg. Kennedy Mpumilwa wameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Meru kutekeleza Ilani ya chama hicho ya mwaka 2022 sura ya pili ibara ya 23 inaelekeza Serikali kuwawezesha wanawake, vijana na watu Wenye Ulemavu ili wajikwamue kiuchumi na kutoa wito kwa vijana kujiwekea akiba kupitia benki ili kukuza mtaji na kujikomboa kiuchumi

Aidha katika Hafla hiyo iliyofanyika makao makuu ya Halmashauri na kuwajumuisha Viongozi ngazi ya Wilaya ,Waheshimiwa madiwani ,wananchi na wanufaika wa Mkopo huo Mhe.Dkt John D. Pallangyo amekabidhi pia, Vyereani vitatu kwa kikundi cha vijana Old is gold youth group toka Usa ambapo vyerehani hivyo ni ufadhili toka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu.



**Julieth Maturo**  
Mwenyekiti wa UWT,Wilay ya Kichama Meru



**Ombeni Mafie**  
Mwenyekiti wa UVCCM,Wilaya ya Kichama Meru



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OR-TAMISEMI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**



**MDAHALO MAALUM KUELEKEA MIAKA**

**61 UHURU**  
**Tanganyika**



**07 Disemba 2022**



**Chuo cha Ualimu Patandi(Tengeru)**



**02:00 Asubuhi**

**AMANI NA UMOJA NI NGUZO  
YA MAENDELEO YETU**

**MGENI RASMI**


**Mhe. Mhandisi Richard Ruyango  
MKUU WA WILAYA YA ARUMERU**

@merudc

[www.merudc.go.tz](http://www.merudc.go.tz)

**“Amani na umoja ni  
nguuzo ya  
maendeleo yetu”**

# DC ARUMERU AHIMIZA UZALENDO KUELEKEA MIAKA 61 YA UHURU



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango ametoa wito kwa Watanzani kuwa wazalendo kwani viongozi waliopigania uhuru wa nchi hii waliweka mbele maslai ya wote ambapo amehimiza ni muhimu kwa Kizazi cha sasa na kijacho kujua thamani ya uhuru na kujengewa nchi kwa kuendelea kuyatunza mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Serikali zote za awamu ya kwanza hadi ya sasa.



# HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU NA MDAHALO KUELEKEA MIAKA 61 YA UHURU



Mhe.Ruyango amesema hayo wakati wa Mdahalo maalum kuelekea Miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, uliofanyika katika ukumbi wa chuo cha Ualimu Patandi ambapo amesema jitihada kubwa za kudai uhuru zilizofanywa na Baba wa Taifa Hayati Mwl.Julius Kambarage Nyerere zililenga kuwa na Taifa huru lenye maendeleo kwa kudhibiti maadui wa tatu ambao ni ujinga, Umaskini na Maradhi.

Ruyango amefafanua kuwa Tanzania imeendelea kupata mafanikio makubwa baada ya Uhuru kwa kupigana dhidi ya maadui hao watatu; ujinga, maradhi na umaskini na kubainisha katika adui wa ujinga Serikali imeongeza wigo wa utoaji wa Elimu, ikikumbukwa wakati wa kupata Uhuru 1961 eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Meru halikuwa na shule hata moja ya Sekondari na kwa sasa zipo Shule 75 za Serikali kati ya shule hizo shule 7 zimesajiliwa katika uongozi wa Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wazee waliokuwepo kipindi cha uhuru wamethibitisha mabadiliko makubwa katika sekta za elimu ,usafirishaji ,afya ,upatikanaji wa huduma za kibenki " tunashuhudia maendeleo kila siku katika nchi yetu ,wito wangu kwa kizazi cha sasa lindeni nchi hii, tunzeni miundombinu iliyopo na kudumisha amani "amesema Gabriel Kaaya ,Askari wa Zamaani na Mshauri wa Jeshi la Akiba

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mhe.Jeremia Kishili ametoa wito kwa Vijana kujituma na kufanya kazi kwa bidii ambapo amewataka vijana kuwa na mtizamo wa kujiajiri.

Mdahalo huo umejumuishia makundi ya viongozi wa Serikali,Dini,Kijamii, Kisiasa ,Wazee maarufu,wananchi na wanafunzi

# MUONEKANO WA JENGO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU KUELEKEA MIAKA 61 YA UHURU WA TANGANYIKA



Jengo la Makao Makuu Halmashauri ya Wilaya ya Meru likiwa limepambwa kuelekea Miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika. Meru tunatambua na kupongeza juhudi za Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere na viongozi wengine katika kupigani Uhuru wa nchi yetu.

**“Amani na umoja ni nguzo ya maendeleo yetu”**

# MKUU WA WILAYA YA ARUMERU AZINDUA AWAMU YA NNE YA UTOAJI WA CHANJO YA POLIO



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango amezindua rasmi kampeni ya awamu ya nne ya chanjo ya Polio itakayofanyika kwa Siku nne kuanzia leo tarehe 01 hadi 4 Disemba 2022, ambapo ametoa wito kwa jamii kuwalinda watoto dhidi ya ugonjwa Polio unaosababisha Kupooza na Ulemavu wa viungo wa kudumu kwa kuhakikisha wanapata chanjo ya Polio.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru Mhe. Ruyango amesema lengo kampeni ya utoaji chanjo ya matone ya polio ni kuongeza kinga mwili kwa Watoto chini ya miaka mitano na hivyo kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Polio ambao uliripotiwa kuwepo nchi ya jirani ya Malawi " Mtoto asiyepata chanjo ni hatari kwa maisha yake na kwa jamii nzima kwani anaweza kuambukizwa au kuwaambukizwa wengine "amehimiza Mhe.Ruyango







MMkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya amesema Serikali inahakikisha Watoto wapo salama kwa kuhakikisha chanjo dhidi ya Polio inatolewa hivyo ametoa wito kwa wazazi ,walezi na jamii kwa ujumla kushiriki kikamilifu kuhakikisha watoto wanapata chanjo.



Mratibu wa chanjo Halmashauri ya Wilaya ya Meru Salome Mbegela amesema katika awamu ya nne chanjo ya polio itatolewa kwa siku nne kuanzia leo tarehe 1 hadi 4 Disemba 2022 ambapo watoto 63,198 wanatarajiwa kupata chanjo ambayo itatolewa nyumba kwa nyumba, vituo vya huduma za afya, vituo vya kulelea watoto, katika shule nk

Vilevile Salome ametoa wito kwa jamii kuendelea kutoa ushirikiano kama ilivyofanya katika awamu za chanjo zilizopita ambapo Halmashauri ya Meru ilifanya Vizuri awamu zilizotangulia ikiwa katika awamu ya pili ya kampeni ya utoaji chanjo ya Polio watoto 54,947 walipata chanjo sawa na alilimia 138.6% na katika awamu ya tatu watoto 63,198 walipata chanjo sawa na asilimia 111.7% na ka

Winirose mbise ambaye ni mzazi mwenye mtoto aliyepata chanjo ametoa wito kwa wazazi wote kushiriki kuwapa watoto chanjo ya Polio kwani ugonjwa huo ni hatari

# WAZAZI KUKOSA MUDA WA KUSIKILIZA WATOTO HUCHANGIA VITENDO VYA UKATILI



Kitendo cha wazazi wengi kuwa na utamaduni wa kukosa muda wa kuwa karibu na watoto, ikiwa ni pamoja na kuwasikiliza. Pia ugomvi baina ya wazazi (baba na mama) imechangia watoto wengi kufanyiwa vitendo vya kikatili na kuwa wasiri hadi pale madhara makubwa yanapotokea.

Hayo yamesemwa na afisa Ustawi Halmashauri ya Wilaya ya Meru Maria Mchallah wakati wa kilele cha kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili kwa wanawake na Watoto katika Halmashauri hiyo, ambapo zaidi ya watoto elfu mbili wamepewa elimu na kujengewa uwezo wa kuwa wajasiri kufichua vitendo vya ukatili.

Mchallah ametoa wito kwa wazazi kuimarisha misingi ya malezi kwani ugomvi na kutengana kwa wazazi inachangia watoto kufanyiwa ukatili na kukosa sehemu ya kusemea.

Mhe.Omari Mshana ambae ni Diwani wa Kata ya Usa-River ambapo kilele cha kampeni hiyo kimefanyika, ametoa wito kwa jamii na Wananchi wote katika halmashauri hiyo kuunga mkono juhudi za serikali katika kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya kikatili



Mhe.Omari Mshana  
Diwani wa Kata ya Usa-River



Wanafunzi wa Shule ya Msingi  
Leganga



Naye, Jane Mandi askari Polisi toka dawati la jinsia Arumeru ametoa wito kwa wananchi kushiriki kikamilifu kupinga ukatili wa kijinsia kwa kufika mahakamani kutoa ushahi Mahakamank kutoa ushahidi ili hatua za kusheria kuchukuliwa kwa watuhumiwa wa vitendo vya kikatili.

Afisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Meru Bi. Flora Msilu amesema suala la kupinga ukatili ni endelevu kila siku ambapo amewashukuru wadau mbali mbali kushirikiana na halmashauri hiyo katika kampeni ya siku 16 ya kupinga ukatili wa kijinsia ambapo elimu imetolewa kwa wananchi na wanafunzi katika kata za kikatiti, Ambureni, Poli na Usa river

Kauli mbiu ya Maadhimisho haya ambapo katika Halmashauri ya Meru yamefanyika katika Shule ya Msingi Leganga ni "KILA UHAI UNATHAMANI, TOKOMEZA MAUAJI NA UKATILI DHIDI YA YA WANAWAKE NA WATOTO"



# ARUMERU, JAMII YAASWA KUJIKINGA DHIDI YA JANGA LA UKIMWI



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango, ametoa rai kwa Jamii kujikinga thidi ya janga la UKIMWI kwa kujiepusha na vitendo vitakavyowapelekea kupata maambuzi ya virusi vya UKIMWI.

Mhandisi Ruyango ametoa rai hiyo katika maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani ambapo kwa Kiwilata h yamefanyika katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Mhe. Ruyango amekemea vikali tabia ya baadhi ya wana jamii kupuuza na kutokuona madhara ya UKIMWI na kujihusisha na vitendo ambavyo vinaweza kupelekea kupata maambukizi hayo

“tafsiri ya maadhimisho ya siku ya UKIMWI ni siku ya kudhibiti UKIMWI inayotumika kutoa elimu kwa jamii wajitambue na wajue kuwa UKIMWI upo, unaua na hauna chanjo wala tiba” amesisitiza Mhandisi Ruyango.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Mwl. Zainab Makwinya, amesema lengo la kufanya maadhimisho katika Taasisi ya Maendeleo ya jamii Tengeru ni kuwafikia vijana ambao ni wanafunzi ambao umri wao ni kuanzia miaka 17 kuendelea ambao wapo katika kundi linaloathirika kwa kiasi kikubwa na maambukizi ya ugonjwa huu.

Aidha, Makwinya amewaelekeza wakuu wa Idara za Afya na Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Meru kuhakikisha Elimu juu ya UKIMWI ni endelevu kwa vijana hao.



Kwa upande wake Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Dkt. Bakari George, ameushukuru uongozi wa wilaya ya Arumeru na Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kuridhia kufanyika kwa maadhimisho haya katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na ameahidi Taasisi hii kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuandaa maadhimisho kama hayo.





Kwa upande wake Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Dkt. Bakari George, ameushukuru uongozi wa wilaya ya Arumeru na Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kuridhia kufanyika kwa maadhimisho haya katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na ameahidi Taasisi hii kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuandaa maadhimisho kama hayo.





Juhudi za awamu ya sita kudhibiti utapia mlo,

Watendaji 26 wa Kata za Halmashauri ya Meru, Wilayani Arumeru wasaini mkataba wa Lishi ikiwa ni juhudi za Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan za kupinga na kuzuia utapiamlo kwenye jamii ikizingatiwa lishe ni msingi wa afya ya binadamu, maendeleo ya jamii na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango wakati wa ufunguzi kikao cha Watendaji cha kusaini mikataba ya lishe, ameelekeza agenda ya lishe kuwa ya kudumu kwenye mikutano kuanzia ngazi za vijiji na Kata ambapo amewataka watendaji hao kushirikiana na watalamu wa lishe kutoa elimu kwa jamii kupitia mikutano sambamba na kuhamasisha jamii kutumia makundi matano ya vyakula.

Mhe.Ruyango amesema Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo imetoa zaidi ya milioni 120 za afua za lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 katika Halmashauri ya Meru hivyo ametoa wito kwa viongozi wa ngazi zote kuunga mkono jitihada hizo za Serikali kwa kusimamia vyema maswala ya lishe kwenye maeneo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya ambaye ameingia Mkataba na watendaji wa Kata 26 za Halmashauri hiyo ametoa wito kwa watendaji na jamii kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa mkataba huo wa lishe unaolenga kuwa na jamii bora ambapo amemshukuru Mhe.Rais kuwa mstari wa mbele latika kuimarisha suala la lishe.



Wakizungumza kwa nyakati tofauti watendaji wa Kata wameahidi kusimamia vyema mikataba hiyo ambapo wameishukuru Serikali kwani mbali na mikataba hiyo imewapa vitendea kazi yaani usafiri utakao wawezesha kuifikia jamii"tunaishukuru Serikali kutupa pikipiki 3 kwa ajili ya ufuatiliaji wa masula ya lische"ameshukuru Elirehema Molel Afisa Mtendaji Kata ya Usa River.

Zoezi hilo la utiaji saini mikataba ya lische limefanyika katika ukumbi wa Halmashauri kushuhudiwa na wakuu wa Idara na Vitengo, Kamati ya uendeshaji huduma za afya ngazi ya Wilaya na baadhi ya wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama Wilaya ya Arumeru





# BENKI YA NMB YAKABIDHI VIFAA TIBA ZAHANATI YA KIKATITI



Benki ya NMB yakabidhi vifaa tiba kwa zahanati ya Kikatiti ikiwa ni kuunga mkono mwamko wa ukamilishaji wa zahanati hiyo uliofanywa na Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan ambapo alichangia milioni 10 za ukamilishaji wa zahanati hiyo wakati akisalimiana na wananchi wa Kikatiti Oktoba 2021.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi vifaa tiba hivyo Meneja wa Benki ya NMB kanda ya Kaskazini Bwn.Dismas Prosper amesema, benki hiyo inaunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya sita katika kuwaletea wananchi maendeleo ambapo imetoa kitanda cha kujifungulia kinamama ,kitanda cha wagonjwa godoro, mzani wa kuwapima uzito wagonjwa, mizani mbili ya kupimia wtoto wanapozaliwa ,stendi za dripu katika zahanti ya kikatiti na katika sekta ya elimu benki hiyo imetoa bati 130 kwa shule ya Sekondari Umoja King'ori hivyo jumla ya michango hiyo ni Shilingi Milioni saba.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru ameipongeza Benki ya NMB kuunga mkono juhudi za Serikali za uboreshaji wa huduma za afya sambamba na miundombinu katika sekta ya elimu ambapo ameendelea kuikaribisha Benki hiyo kuendelea kushirikiana na Serikali kuwaletea maendeleo wananchi "leo tumeshuhudia wananchi hawa wa Kikatiti wakituma salamu za shukrani kwa Mhe .Rais , tunaipongeza NMB kuunga mkono hamasa hii ya Mhe.Rais"amesema mhe Ruyango

# BENKI YA NMB YAKABIDHI VIFAA TIBA ZAHANATI YA KIKATITI



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya ameishukuri Benki ya NMB ikiwa ni mdau wa pili kuunga mkono ukamilishaji wa zahanati ya Kikatiti baada ya Shirila la Cross Talent Share International (CTSI) kuchangia milioni 135.38 hadi sasa katika ukamilishaji wa zahanati hiyo.

Makwinya amesema baada ya Mhe.Rais kuchangia Milioni kumi za ukamilishaji wa zahanati ya kikatiti, hamasa ilianza na Halmashauri ilichangia milioni 10 na Mbunge kupitia mfuko wa jimbo alichangia Milioni 5 ambapo mwamko huo umeendelea kwa wadu wa CTSI na NMB





Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya ameishukuri Benki ya NMB ikiwa ni mdau wa pili kuunga mkono ukamilishaji wa zahanati ya Kikatiti baada ya Shirila la Cross Talent Share International (CTSI) kuchangia milioni 135.38 hadi sasa katika ukamilishaji wa zahanati hiyo.

Makwinya amesema baada ya Mhe.Rais kuchangia Milioni kumi za ukamilishaji wa zahanati ya kikatiti, hamasa ilianza na Halmashauri ilichangia milioni 10 na Mbunge kupitia mfuko wa jimbo alichangia Milioni 5 ambapo mwamko huo umeendelea kwa wadu wa CTSI na NMB



Meneja wa Benki ya NMB kanda ya Kaskazini Bwn.Dismas Prosper



JAMHURI YA  
MUUNGANO  
WA TANZANIA

WIZARA YA  
KATIBA NA  
SHERIA



# KAMPENI YA UTOAJI WA MSAADA WA KISHERIA KWA WANANCHI

31 Oktoba hadi 02 Novemba 2022

Saa 3:00 Asubuhi

Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Ngarenanyuki

## MAMBO YATAKAYOFANYIKA

Mada kuhusu Sheria mbalimbali

Kusikiliza watu wenye mahitaji  
au migogoro ya kisheria

Ushauri wa Kisheria, Usuluhishi na  
upatanishi

Kusaidia wahitaji Kuandaa  
nyaraka za Kisheria.

## KAULI MBIU

“Utatuzi Wa Migogoro  
Kwa Njia Mbadala  
Hupunguza Uadui na  
Kuzuia Umaskini”

## WASHIRIKI

MAWAKILI WA SERIKALI, MAWAKILI WA  
KUJITEGEMEA, MAAFISA ARDHI NA  
WANASHERIA WA HALMASHAURI, MAAFISA  
USTAWI WA JAMII, WASAIDIZI WA KISHERIA

## WADAU WENGINE

MAHAKAMA, JESHI LA POLISI, RITA

## AWAMU YA SITA KAZINI

Serikali ya awamu ya sitaikiongozwa na Dkt.Samia Suluhu Hassan kupitia wizara ya katiba na sheria imeendelea kuhakikisha inatutua changaoto mbalimbali zinazowakabili wananchi ikiwa ni utatuzi wa migogoro njia mbadala ili kuharakisha maendeleo

## UZINDUZI WA KAMPENI YA MSAADA WA KISHERIA NA UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA MBADALA



Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Wilayani Arumeru wameishukuru Serikali ya awamu ya sita ambapo kupitia kampeni ya siku tatu ya utoaji msada wa kisheria na usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala inayowezesha na wizara ya katiba na sheria wameanza kunufaika .

Akizindua kampeni hiyo inayodumu kwa siku tatu, Mwl. James Mchembe ambaye ni katibu Tawala Wilaya ya Arumeru akimwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo, amesema serikali ya awamu ya sita imeendelea kuhakikisha wananchi wasio na uwezo wa kumudu gharama za mawakili wanasaidika kwa mujibu wa sheria ya utoaji msaada wa kisheria ya mwaka 2017 ambapo amewataka wananchi kujitokeza katika kampeni inayoendelea katika Kata ya Ngarenanyuki ya utoaji msaada wa kisheria.

Mwl. Mchembe amewataka wataalumu katika kampeni hiyo kuwahudumia wananchi kwa weledi ili kampeni kuwa na tija "wasikilizeni wananchi ili muelewe changamoto zao na kuwasaidia" amehimiza Mwl. Mchembe

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Meru Mwl. Zainabu Makwinya amesema kampeni hiyo ni fursa kwa wananchi kupata uelewa na msaada wa kisheria sambamba na kujua taratibu mbalimbali "katika kampeni hii mbali na uwepo wa mabanda ya msaada wa kisheria pia uelewa na elimu ya masuala mbalimbali inatolewa mfano tuna banda la Maendeleo ya Jamii linaelimisha juu ya taratibu za kupata mkopo usio na riba unaotolewa na Halmashuri" amefafanua Makwinya



Naye Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Meru, ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Ngarenanyuki Mhe. Aminiel Mungure kwa niaba ya wananchi ameishukuru Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusogeza huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi na kuomba Serikali kuendelea kutatua Migogoro ya Ardhi iliyopo ikiwemo ya ngazi za Mikoa na Wilaya.

Laurent Burilo ambaye amemwakilisha Msajili wa mashirika yanayotoa msaada wa kisheria Wizara ya Katiba na Sheria amesema sheria ya utoaji msaada wa huduma za kisheria ya mwaka 2017 inalenga kutimiza azma ya serikali ya kuondoa migogora na kuendeleza amani ambapo ametoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kupata elimu na huduma bila gharama



## UTAMBULISHO MRADI WA KIZAZI HODARI UNAOTEKELEZWA NA KANISA LA KKKT



Kanisa la Kiinjili la Kirutheli Tanzania ( KKKT) kanda ya Kaskazini Mashariki Naibu Mkurugenzi wa Mradi huo Bi.Vaileth Mollel amesema mradi wa Kizazi Hodari unafadhiliwa na Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani USAID ni wa miaka mitano na unalenga kuwafikia wanufaika 7162 ambao ni watoto yatima ,watoto walio katika mazingira hatarishi na kaya zao pamoja na vijana wa rika balehe katika Halmashauri za Meru na Arusha Jiji .

Mollel amesema lengo kuu la Mradi wa Kizazi Hodari ni kuimarisha afya ,ustawi na ulinzi kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi (OVC), vijana walioathiriwa na VVU na walezi wao ili kufikia malengo ya dunia ya kupambana na VVU kwa asilimia 95%,95%,95% kwa mchanganuo wa 95% kupima na kufahamu hali ya maambukizi ya VVU ,95% ya waliopima na kukutwa na maambukizi kuanza kutumia dawa na 95% ya wanaotumia dawa kutumia dawa kwa ufasaha na kufubaza VVU

Awali akifungua kikao hicho cha utambulisho wa Mradi Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mhe.Jeremia Kishili amesema Serikali inaendelea kushirikiana na wadau kuwaletea wanachi maendeleo ambapo ameshukuru uwepo wa mradi wa Kizazi hodari na kutoa wito mradi huo kuwagusa waliolengwa/waliokusudiwa.

Naye Meneja Mradi wa Kizazi Hodari Kanda ya Kaskazini Bwn. Aminieli Mongi amesema mradi wa Kizazi Hodari kanda ya Kaskazini Mashariki unatekelezwa katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro,Tanga Manyara ,Singida Dodoma na Morogoro uki fadhiliwa na Shirika la USAID na mtelelezaji Mkuu ni Kanisa la Kiinjilisti la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambapo mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri 26 ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Meru .

# UZINDUZI WA ZOEZI LA AUTOAJI DAWA ZA MINYOO KWA WATOTO UMRI MIAKA 5 HADI 14



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhe, Mhandisi Richard Ruyango, amezindua rasmi zoezi la kumzesha dawa za kinga tiba dhidi ya Minyoo kwa watoto umri 5 hadi 14 katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru ambapo ameelekeza zoezi hilo kufanyika kwa ufanisi mkubwa ili kuwa na tija .

Mhe.Ruyango amefanya uzinduzi wa zoezi hili kwa Halmashauri katika shule ya msingi Leganga kata ya Usa River ambapo zoezi hilo litaendelea katika shule zote za msingi za Halmashauri ya Meru kwa watoto wenye umri wa miaka 5 mpaka 14.

Halmashauri ya Meru inategemea kutoa kinga tiba ya minyoo kwa watoto 67,000. Watoto 62,000 kati yao ni wale waliosajiliwa shuleni na watoto 5,000 ni ambao hawajasajiliwa kwenye mfumo rasmi wa elimu.

Dawa tiba hiyo inatolewa kwenye shule za msingi 173 ambapo wagawa dawa ni walimu 346 waliopata mafunzo wakisimamiwa na watoa huduma za afya 124 walioko kwenye kata zote.





# WAKULIMA WA MBOGAMBOGA NA MATUNDA WATAKIWA KUJIUNGA NA USHIRIKA



Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, imewahamasisha wakulima wa mboga mboga na matunda kujiunga na vyama vya Ushirika ili kuleta tija katika shughuli za uzalishaji na kujikwamua kiuchumi.

Ushauri huo umetolewa na Ndimolwo Laizer kutoka Tume ya Maendeleo Ushirika wakati wa utoaji wa elimu ya uhamasishaji kwa wakulima wa Mbogamboga wa vikundi vya Nkoamala na Jikomboe vilivyopo katika Kata ya Nkoanrua katika Halmashuri ya Wilaya ya Meru, MKoani Arusha.

Uhamasishaji huo umefanyika tarehe 14 Novemba 2022 ambapo Bw. Ndimolwo Laizer ametoa wito kwa wakulima hao kuunda Ushirika ili kilimo hicho kiweze kuleta tija zaidi na kujikwamua zaidi kiuchumi.

"Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imeanzisha Programu ya uhamasishaji kwa wakulima wa mbogamboga kuunda Vyama vya Ushirika katika Mikoa mitatu ya Tanzania Bara, ambayo ni Arusha, Njombe na Mbeya. Katika Mkoa wa Arusha zoezi hili limeanza katika Halmashauri ya Meru na itaendelea katika Halmashauri za Arusha Vijijini na Karatu," alisema Laizer. Aidha, Bw. Laizer

Laizer ameeleza miongoni mwa manufaa ya Vyama vya Ushirika kwa wakulima wa mboga mboga ni pamoja na kupanua mtaji na kuimarisha nguvu ya kiuchumi kwa mkulima, kurahisisha upatikanaji wa masoko ya mazao na bidhaa, pamoja na upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa bei nafuu.

Nao wakulima wa mbogamboga wameishukuru Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kukipa kipaumbele kilimo cha mbogamboga ambapo wameomba elimu hiyo kuwa endelevu ili kuwafikia wakulima wengi zaidi

# ZOEZI LA UWEKAJI MIFUGO HERENI ZA KIELETRONIKI.



Halmashauri ya Wilaya Meru imeendelea kuwahamasisha wafugaji kuhakikisha mifugo yao inawekwa na hereni za kielekroniki kwani kunafaida uwekaji hereni za kielekroniki kwa mifugo ambazo ni pamoja na hakika wa soko la mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi, kuwezesha Serikali na Wadau kuweka mipango madhubuti ya kuboresha huduma za mifugo, Kudhibiti wizi wa mifugo, kusaidia kukabiliana na magonjwa ya mlipuko nk



# UHAMASISHAJI MAZOEZI/MICHEZO KWA AFYA



Halmashauri ya Wilaya ya Meru kupitia kitengo cha utamaduni na michezo imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhamasisha michezo na mazoezi kwa afya.

## MASHINDANO YA LADRUN

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl.Zainabu Makwinya ni miongoni mwa washindi ambao wametunikiwa medali ya mbio za umbali wa km 10 katika mashindano ya mbio Maalum za kuzunguka Ziwa Duluti ikiwa ni kuhamasisha utalii wa ndani pamoja na ufanyaji mazoezi ya viungo.

Mashindano hayo yameratibiwa na Mkurugenzi wa Oldonyo Lengai Adventure yamefanyika leo tarehe 18 Disemba 2022, na kujumuisha washiriki toka ndani na nje ya Mkoa wa Arusha.



# UZINDUZI WA MATOKEO YA AWALI YA SENSA YA WATU NA MAKAZI



## 61,741,120

**TAREHE 31 OKTOBA 2022**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, DKT.Samia Suluhu Hassan alitangaza kuwa Tanzania ina idadi ya watu 61,741,120 ambapo watu 59,851,347 wapo Tanzania Bara na watu 1,889,773 wapo Zanzibar.

Kati ya watu 61,741,120, wanawake ni 31,687,990 sawa na asilimia 51 na wanaume ni 30,053,130 sawa na asilimia 49. Kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita Tanzania ilikuwa na watu 44,928,923, hivyo kuna ongezeko la watu 16,812,197 sawa na ongezeko la asilimia 3.2 kwa mwaka kati ya mwaka 2012 na mwaka 2022.

Mhe.Dkt Samia alitoa wito kwa viongozi wa Serikali kuanza kutumia matokeo ya Sensa katika kupanga miradi na mipango jumuishi ya maendeleo endelevu kwa wananchi.



# KAZI IENDELEE.....



**Mhe Jeremia Kishili**

Kiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru

**Mhandisi Richard Ruyango**

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru

**Mwl Zainabu J. Makwinya**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya  
Wilaya ya Meru

## ZALENDO

Ushirikiano na mshikamano uliopo kwa viongo ngazi zote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Uongozi wa Wilaya ya Arumeru na Uongozi ngazi ya Mkoa wa Arusha umeleta tija katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, ikikumbukwa kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chama kinachushinda uchaguzi Mkuu ndicho kinacho unda Serikali.


Mafanikio katika sekta ya elimu, afya, maji, miundombinu ya barabara ni matokeo ya kujikita kwenye misingi ya ilani ya CCM inayohimiza uzalendo kwa nchi ndio msingi wa maendeleo ya kweli ya Tanzania ambayo yataletwa na Watanzania wenyewe kwa kuwa wazalendo kutekeleza majukumu yao pale wanaposhika nyazifa mbalimbali, Vilevile wananchi kutunza na kuyaenzi maendeleo kwa kuitunza miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kwenye maeneo yao.




Uongozi wa Halmashauri ya  
Wilaya ya Meru unawatakiwa  
Wataanzania wote  
Kheri ya Mwaka mpya

2023

Tusherekee kwa Amani na  
kazi iendeleee....







*Theri ya*  
*Mwaka mpya*  
**2023**



Mhandisi Richard Ruyango  
Mkuu wa Wilaya ya Arumeru






Mhe. Jeremia Kishili  
Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Meru

*Theri ya*  
*Mwaka mpya*  
**2023**

**HAPPY**  
*New Year*







*Theri ya*  
*Mwaka mpya*  
**2023**



Mwl. Zainabu Makwinya  
Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Meru

**HAPPY**  
*New Year*





Asante msomaji wa "Jarida la FAHARI YETU HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU",

msomaji wetu Halmashauri ya Wilaya ya Meru Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini inaendelea kuhakikisha umma unapata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za serekali, ushiriki wa wadau mbalimbali kwenye swala la maendeleo, ambapo itaendelea kukuletea jarida hili "FAHARI YETU HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU" kila baada ya robo (miezi mitatu) ya mwaka wa fedha 2022/2023



merudistrictcouncil2



@meru



www.merudc.go.tz

JARIDA

FAHARI

1

2

2 2 2 2 2 2 2 2  
2 2 2 2 2 2 2 2  
2 2 2 2 2 2 2 2  
2 2 2 2 2 2 2 2